# Usifiwe, utukuzwe milele

**Zaburi ya siku ya Mungu ya Utatu utakatifu, Mwaka A**
**Dan. 3, 52, 53-54, 55-56**

Eugène AMPIRE Bisimwa




1. Utukuzwe, ee Bwana, Mungu wa baba zetu,
Usifiwe, utukuzwe milele.
Likuzwe jina lako tukufu na takatifu,
Lisifiwe, litukuzwe milele.

2. Ukuzwe katika hekalu lako tukufu na takatifu,
Uimbwe, utukuzwe juu ya yote milele.
Ukuzwe katika kiti cha ufalme wako,
Usifiwe, uimbwe juu ya yote milele.

3. Ukuzwe unayepima vilindi, unayekaa juu ya makerubi,
Usifiwe, utukuzwe juu ya yote milele.
Ukuzwe katika anga la mbingu,
Uimbwe, utukuzwe juu ya yote milele.